# I.Habari kuhusu bidhaa

# Mada ya 19

# Mgawanyo wa mbegu

# JARIDA LA UHAKIKA

## I. Habari kuhusu bidhaa

## <u>Mada ya 19:</u> Mgawanyo wa mbegu

Kuna aina mbili kuu za mbegu zinazopatikana katika bara la Afrika.

**Uhifadhi wa mbegu kutoka shambani**
Kuhifadhi mbegu kutoka shambani ili kupanda katika msimu unaofuata ndiyo njia rahisi na isiyo na gharama ya juu kwa mkulima. Mkulima huhifadhi sehemu ya mavuno/mazao ili kupanda katika msimu ufuatao. Mbegu hizi huwa hazijafanyiwa uchanganuzi, hazijaoshwa wala kutibiwa.

Ingawa kuhifadhi mbegu kutoka shambani ni njia isiyokuwa na gharama, upo upungufu mwingi sana:

- Hakuna udhibiti wa **ubora wa mbegu**. Ubora wa mbegu waweza kuwa wa hali ya juu kwa msimu mmoja na wa hali ya chini kwa misimu mwingine.
- **Magonjwa** kama kuvu yaweza kuhamishwa kutoka msimu mmoja hadi mwingine.
- Mbegu hizi **hazijaoshwa.** Uwezekano wa mbegu za magugu kumea/kukua kati ya mimea ya mazao ni wa juu.
- Mbegu **hazijafanyiwa uchanganuzi** katika majaribio shambani ili kuamua asilimia ya mbegu itakayo ota na usafi wa mbegu.
- Mbegu huhifadhiwa shambani na mkulima mpaka msimu ufuatao. Hii husababisha kupotea kwa mbegu kwa kuharibiwa na wadudu waharibifu.
- Mbegu huhifadhiwa bila kujali kiwango cha unyevu. Mbegu zilizo na unyevu mwingi huoza wakati wa kuhifadhiwa na mbegu chache tu ndizo huota, jambo ambalo husababisha upungufu wa mavuno/mazao.

Sio mbegu zote zilizohifadhiwa kutoka shambani zina upungufu huu. Kuna baadhi ya wakulima walio na miradi ya kuhifadhi mbegu ambapo mbegu hupimwa au hufanyiwa uchanganuzi, kusafishwa na kutibiwa. Mbegu hizi hudumisha asimilia ya juu ya uotaji na pia mavuno/mazao ya juu.

**Mbegu zilizothibitishwa/mbegu halali**
Mbegu zilizothibitishwa ni mbegu za ubora wa hali ya juu na ukuzaji mkuu zilizozalishwa kwa uthabiti halisi na wastani. Waoteshaji mbegu walio hitimu huzalisha mbegu halali. Mbegu hizi ni za bei ghali kuliko mbegu ambazo hazijathibitishwa lakini zina faida/manufaa yafuatayo:

- Mbegu zilizothibitishwa huzalishwa kwa njia halisi ya wastani ya uthibitishaji wa mbegu.

- Zina thibitisho ya uwezo wa kuota.
- Mbegu zilizothibitishwa huondolewa uchafu na hufikisha kiwango fulani cha mbegu magugu au mbegu tepetevu.
- Kiwango cha unyevu wa mbegu zilizothibitishwa hupimwa kabla kuhifadhiwa ghalani.
- Matarajio ya mavuno/mazao yanaweza kupimwa.
- Mbegu zilizothibitishwa lazima zipite kiasi fulani cha vipimo/uchanganuzi kabla ya kuthibitishwa.

Mbegu zilizothibitishwa/halali ndizo mwanzo wa matokeo ya mazao bora. Manufaa makuu matano ya mbegu zilizothibitishwa kwa wakulima ni:

- Wakulima hupata mbegu safi.
- Wakulima hupata jeni mpya kwa uimarishaji wa mbegu.
- Wakulima hupata mavuno/mazao ya juu.
- Wakulima huwa na utulivu wa mawazo – kwa sababu hasara ni kidogo sana kwa mazao.
- Wakulima hutumia teknolojia ya kisasa ya mbegu.

| |
|---|
| **Kwa kuuza mbegu zilizothibitishwa/halali, wachuuzi wa bidhaa za kilimo hujenga uhusiano wa kuaminiana na wakulima. Watarudi tena na tena.** |

# MAELEZO YA ZIADA


## I. Habari kuhusu bidhaa

## <u>Mada ya 19:</u> Mgawanyo wa mbegu

Kuna hatua kadhaa katika ustawishaji wa aina bora za mbegu:

- **Mbegu za Mwanzo/mbegu zalishi**: Mbegu za mwanzo huzalishwa na mzalishi katika hali inayohakikisha sifa fulani za zao zinaendelezwa.
- **Mbegu kabla ya zile za kimsingi au za msingi**: Mbegu hizi ni kizazi cha mbegu za mwanzo na huzalishwa chini ya uangalifu wa mzalishi au shirika lililoteuliwa na mzalishi.
- **Mbegu za kimsingi/zilizosajiliwa:** Mbegu za kimsingi pia huzalishwa na mzalishi au shirika lililoteuliwa na liko chini ya uangalizi wa sharika la udhibiti wa ubora wa mbegu. Mbegu ya kimsingi husambazwa kwa wakulima walioafikiana na shirika la mbegu ili waweze kuzalisha na kuzidisha mbegu.
- **Mbegu iliothibitishwa/mbegu halali**: Mbegu zinazokuzwa na wakulima walio na kandarasi kutoka kwa mbegu za kimsingi au zilizosajiliwa hukaguliwa na shirika la udhibiti wa ubora wa mbegu kuhusu usafi, uotaji, na kadhalika. Kama mbegu zinatosheleza au kupitisha matakwa/mahitaji hayo basi zitathibitishwa kama halali. Mbegu zote halali huwekwa kitambulisho kwenye pakiti ili kuonyesha kwamba zimekaguliwa. Mbegu zilizothibitishwa/halali zinaweza kutumika kwa uzalishaji wa mbegu au kusambazwa kwa wakulima ili kuzitumia kupanda mimea/mazao.

**Njia ya kufikia mbegu zilizothibitishwa/halali:**



# MWONGOZO

## I. Habari kuhusu bidhaa

## **Mada ya 19:** Mgawanyo wa Mbegu

### Vifaa vinavyohitajika:

- ☑ Ubao ulio na makaratasi
- ☑ Markers (1 nyeusi, 1 bluu, 1 kijani, 1 nyekundu)
- ☑ Kadi za rangi
- ☑ Karatasi kubwa

**Muda unaohitajika:** Dakiki 45

**Maandalizi:**

- ☑ Karatasi za kufungua kurasa zilizo na kichwa: *Mgawanyo wa mbegu.*
- ☑ Kadi mbili za rangi zilizo na maandishi yafuatayo
  - *Mbegu zilizohifadhiwa kutoka shambani*
  - *Mbegu zilizothibitishwa/halali*
- ☑ Kadi kumi na nane (18) zilizo na maandishi yafuatayo:
  - *Mbegu ambazo hazijatibiwa*
  - *Mbegu zisizo safi*
  - *Uwepo wa kiasi cha juu cha mbegu za magugu*
  - *Uwepo wa kiasi cha juu cha mbegu tepetevu*
  - *Ugeukajigeukaji wa ubora wa mbegu*
  - *Kutochanganua mbegu shambani*
  - *Unyevu wa mbegu haujulikani*
  - *Kiwango cha asilimia ya uotaji hakijulikani*
  - *Bei nafuu*
  - *Mbegu zimetibiwa*
  - *Mbegu ni safi*
  - *Uwepo wa kiasi cha chini sana cha mbegu za magugu*
  - *Uwepo wa kiasi cha chini sana cha mbegu tepetevu*
  - *Uwepo wa kila mara wa mbegu za ubora wa juu*
  - *Mbegu zilizopita majaribio/uchanganuzi shambani*
  - *Kiwango cha unyevu kilichodhibitiwa*

- *Kiwango cha asilimia ya uotaji kinachojulikana*
- *Bei ghali*

# Mwanzo

| | |
|---|---|
| **U**sikivu: | Uliza washiriki kama wanajua tofauti kati ya daraja la kwanza na la kumi na mbili shuleni. Watajibu kwamba Daraja la kwanza ndio mwaka wa kwanza wa mtoto shuleni na Daraja la kumi na mbili ndio mwaka wa mwisho shuleni |
| **K**ichwa: | Waambie washiriki kichwa huku ukiwaonyesha karatasi ya kufungua kurasa ilio na kichwa: *Mgawanyo wa mbegu.* |
| **K**usadikika: | Elezea uzoefu wako katika uwanja wa mbegu. |
| **M**alengo: | Kuelezea migawanyo tofauti ya mbolea na faida ya kila aina/mgao. |
| **M**anufaa: | Kuelewa tofauti kati ya migawanyo miwili mikuu ya mbegu itakusaidia katika kuwashauri wateja kuhusu mbegu ilio bora kwa upanzi. |
| **M**welekeo: | Katika kipindi hiki, tutaangazia mgawanyo wa mbegu. Tutaangalia migao miwili mikuu na kufuatia na manufaa/faida na upungufu wa kila mgao. |

# Wasilisho

## **U**fafanuzi, **M**aonyesho, **M**azoezi, na **M**wongozo:

1. Uliza washiriki ni vipi mtoto huendelea shuleni kutoka daraja moja hadi lingine. Waelekeze kujibu ifuatavyo. Wanahitaji kupita mtihani au majaribio. Waeleze kwamba mbegu pia zinahitaji kupita majarabio ili ziweze kuthibitishwa/kuhalalishwa.
2. Waonyeshe washiriki zile kadi mbili zenye maadishi: *mbegu zilizohifadhiwa kutoka shambani* na *mbegu zilizothibitishwa/halali*. Bandika kadi hizo ukutani zikikaribiana.
3. Uliza washiriki maana ya maneno “**mbegu zilizohifadhiwa kutoka shambani**”. Waelekeze kwa jibu: Hizi ni aina za mbegu zilizohifadhiwa kutoka msimu uliopita ili kutumiwa kwa upanzi katika msimu mpya ufuatao. Waambie kwamba mtindo huu umetumika barani Afrika kwa karne nyingi.
4. Uliza washiriki maana ya maneno “**Mbegu zilizothibitishwa/halali**” na uwaongoze kupata jibu. Hizi ni mbegu zilizokuzwa na viwanda vya mbegu ili kuimarisha aina ya mimea/mazao. Mbegu hupimwa na kuthibitishwa kupitia kundi la masharti. Waambie huu ni mtindo wa kawaida duniani.
5. Changanya kadi zile kumi na nane za rangi.

6. Gawanya washiriki katika vikundi vitatu. Patia kila kikundi kadi sita. Waambie kwamba kadi hizi zinahusika na mbegu zilizothibitishwa au mbegu zilizohifadhiwa kutoka shambani. Washiriki wajadiliane ni kadi ipi kati ya kadi hizo **inahusika** na mojawapo ya **migao miwili ya mbegu**. Waambie pia wajadili maana ya maneno/maandishi yalio kwenye kadi za rangi. Kubali muda fulani kwa mjadala huu.
7. Wacha washiriki wabandike kadi hizo chini ya kichwa kinachofaa.
8. Jadili kadi hizo moja baada nyingine na ukiulize kikundi kilichoweka kadi hiyo kufafanua. Uliza vikundi vingine kama vinakubaliana na mahali ambapo kadi hiyo ilibandikwa. Kama kila mtu anakubaliana endelea na kadi nyingine hadi zote zikamilike.
9. Majibu yanatakikana yawe yafuatayo:

    **a. Mbegu zilizohifadhiwa kutoka shambani**

    i. Mbegu ambazo hazijatibiwa
    ii. Mbegu zisizo safi
    iii. Uwepo wa kiasi cha juu cha mbegu za magugu
    iv. Uwepo wa kiasi cha juu cha mbegu tepetevu
    v. Ugeukajigeukaji wa ubora wa mbegu
    vi. Kutochanganua mbegu shambani
    vii. Unyevu wa mbegu haujulikani
    viii. Kiwango cha asilimia ya uotaji hakijulikani
    ix. Bei nafuu

    **b. Mbegu zilizothibitishwa/halali**

    i. Mbegu zimetibiwa
    ii. Mbegu ni safi
    iii. Uwepo wa kiasi cha chini sana cha mbegu za magugu
    iv. Uwepo wa kiasi cha chini sana cha mbegu tepetevu
    v. Uwepo wa kila mara wa mbegu za ubora wa juu
    vi. Mbegu zilizopita majaribio/uchanganuzi shambani
    vii. Kiwango cha unyevu kilichodhibitiwa
    viii. Kiwango cha asilimia ya uotaji kinachojulikana
    ix. Bei ghali

10. Uliza washiriki kueleza ni kwa nini mbegu zilizothibitishwa/halali ni za **bei ghali sana.** Hii ni kwa sababu zimepimwa/zimefanyiwa uchanganuzi. Waulize ni mgao upi wa mbegu ulio bora katika **uzalishaji wa chakula wa kuendelezwa barani Afrika**. Hizi zitakuwa mbegu zilizothibitishwa. Kwa nini? Kwa sababu mavuno/mazao yatakuwa ya juu.

# Malizia

**M**uhtasari: Peana muhtasari ukitumia kadi za rangi.

**M**aswali: Uliza kama kuna yeyote aliye na swali au maoni.

**T**athmini: Uliza washiriki kutaja tofauti tatu kati ya mbegu zilizohifadhiwa kutoka shambani na mbegu zilizothibitishwa/halali.

**H**atua fuatilizi: Katika kipindi hiki, tumejifunza kuhusu migao miwili mikuu ya mbegu na umuhimu wa kila mgao kwa mkulima. Katika kipindi kifuatacho, tutajadili sifa za mbegu.

Sambaza **makaratasi ya taarifa ya maelezo** kwa washiriki wote.